SAVINGS AND CREDIT CO-OPERATIVE UNION LEAGUE OF TANZANIA

SCCULT (1992) LTD

MPANGO WA ELIMU NA MAFUNZO KWA MWAKA 2021

Imeandaliwa na;

IDARA YA UJENZI WA UWEZO

CHAMA KIKUU CHA USHIRIKA

WA AKIBA NA MIKOPO TANZANIA

SCCULT (1992) LTD,

S.L.P 20640, Dar es Salaam, Tanzania

Simu: +255 222 185 548/9

Barua pepe: info@sccult.com/training@sccult.com



“SCCULT JUMUISHI KWA USTAWI WA SACCOS.”

YALIYOMO

Salamu za Mwenyekiti 1
Salamu za Katibu Mtendajii 2

1.0 Utangulizi 3
1.1 Dira/ Maono ya SCCULT (1992) LTD 3
1.2 Dhamira/Dhima 4
1.3 Kauli Mbiu 4
1.4 Maadili 4

2.0 Kazi na Wajibu wa SCCULT (1992) LTD 4

3.0 Aina za Mafunzo (Type of Training) 5
3.1 Mafunzo ya Darasani 5
3.2 Mafunzo Kazini (On job trainings) 5
3.4 Mafunzo Maalum (Taller made) 5
3.5 Mafunzo Shirikishi (Participatory) 6
3.6 Ziara za Kimafunzo ndani ya Nchi 6
3.7 Ziara ya kimafunzo nje ya Nchi 6

4.0 Mbinu na Njia za Uwezeshaji 6
4.1 Matumizi ya Darasa 6
4.2 Kazi za Vikundi 7
4.3 Michezo, Maigizo na visa mkasa 7

5.0 Matarajio 8

6.0 Tathmini ya Mafunzo (Training Need Analysis) 8

7.0 Kalenda ya Mafunzo Mwaka 2021 8

Dkt. Gervas M. Machimu

SALAMU ZA MWENYEKITI

Kwa niaba ya Bodi ya uongozi wa Chama Kikuu cha Ushirika wa Akiba na Mikopo Tanzania SCCULT (1992) Ltd, napenda kuchukua fursa hii kuwasalimu kwa upendo na kuwashukuru kwa namna mlivyokubali kuwa sehemu ya historia mpya ya SCCULT (1992) Ltd yenye kubeba maono makubwa na malengo ya kuboresha Sekta ya Ushirika wa akiba na mikopo Nchini.

Shukrani za pekee ziwaendee wasimamizi wetu Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) na msimamizi Mkuu Benki Kuu ya Tanzania (BOT), Shirikisho la vyama vya ushirika Tanzania (TFC), Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU), Shirika la ukaguzi na usimamiz wa vyama vya ushirika (COASCO), Shirikisho la vyama vya ushirika wa akiba na mikopo Afrika (ACCOSCA) pamoja na vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo SACCOS wanachama na wasio wanachama.

Aidha, ninawashukuruku wadau wetu kama Saving Banks Foundation for international Cooperation (SBFIC) kwa ushirikiano wameouonesha katika katika shughuli mbalimbali za SCCULT (1992) Ltd na wanachama wake. Nipende kuwahakikishia kuwa SCCULT (1992) Ltd tumekusudia kutoa huduma bora za mafunzo na ushauri wa kitalaamu kwa SACCOS kwa viwango stahiki ili kuwezesha SACCOS kuwa shindani, kuboresha uendeshaji wake katika soko huru la fedha. Kwa mwaka 2021, SCCULT (1992) Ltd imejipanga kuboresha Mifumo yake ya ndani, uwezo wa rasilimali watu, mahusiano na wadau wake na kuongeza mtandao wa washirika na watalaamu ndani na nje ya Nchi kwa lengo la kuendelea kutoa huduma bora, zinazoendana na mahitaji ya vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo lakini pia kuwezesha mabadiliko chanya na ya haraka kwa SACCOS yanatokana na mabadiliko ya mazingira ya soko la huduma za fedha.

Wito wangu kwa Wanachama, Viongozi, na watendaji wa vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo SACCOS ni kuwasihi watambue umuhimu wa elimu kuwa ndio nyezo kuu ya kuwawezesha kuongeza stadi, ujuzi na kutengeneza mahusiano ya kisekta ambayo yatasaidia kubadilishana uzoefu kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu utendaji wa SACCOS. Natoa wito wana SACCOS kuhakikisha tunatimiza vema msingi huu namba 5 wa ushirika unaohusu Elimu, Mafunzo na taarifa na SCCULT (1992) Ltd ni sehemu sahihi kuhakikisha tunaishi msingi huo

Hassani S. Mnyone

SALAMU ZA KATIBU MTENDAJI

Ndugu wana SACCOS na wadau wote wa Sekta ya ushirika Tanzania natoa salaamu na kuwashukuru wote mliofanikisha kwa kiasi kikubwa mpango wetu wa mafunzo kwa mwaka 2020. Nashukuru sana Viongozi waliokuwa wakishiriki kufungua au kufunga Semina zetu ambazo tulikuwa tukiziendesha katika Mikoa na Wilaya mbalimbali Nchini.

Pia tunawashukuru sana wadau wetu ambao ni wawezeshaji wanaotoka nje ya SCCULT (1992) Ltd toka asasi na idara za Serikali ambazo ni wadau wa ushirika kama TCDC, MoCU, COASCO, TRA, BOT. Aidha niwashukuru na wadau wetu wengine ambao kwa kiasi kikubwa wameamua kuwekeza SCCULT (1992) Ltd kuhakikisha huduma za Mafunzo na huduma nyingine zinaboreshwa kufikia viwango vya kimataifa na kuwa na tija kwa washiriki, wadau hao ni kama SBFIC, ACOSCA, pia tunawashukuru sana baadhi ya watendaji kutoka kwenye SACCOS ambao walikuwa sehemu ya wawezeshaji wetu, na wawezeshaji binafsi. Aidha tunazishukuru pia Mamlaka za Halmashauri za Wilaya, Mikoa na Manispaa mbalimbali kwa michango yao ya kuwezesha mafunzo yetu kufanyika katika viwango na ubora mzuri. Tunaomba nyote muendelee kuwa nasi na kutuunga mkono mwaka 2021.

Napenda kuwataarifu kuwa mwaka 2021 tumejipanga kuwahudumia vizuri zaidi katika kuwapatia mafunzo, elimu na habari kwa ubora mkubwa kwenye maeneo mbalimbali kama uongozi, uendeshaji na usimamizi wa SACCOS. Zipo bidhaa mpya katika mpango wetu wa elimu na mafunzo kwa 2021 na kuufanya mpango kuangalia mambo ya kisasa zaidi, mahitaji na mabadiliko yanayojitokeza katika shughuli za SACCOS hasa katika teknolojia, masoko na mazingira ya ushindani.

Tunawaomba sana wana SACCOS wote na wadau wote kutuunga mkono ili kuhakikisha tuna timiza malengo yetu tuliyojiwekea kupitia mpango huu na mipango mingine ya SCCULT (1992) Ltd kwa mwaka 2021.

Nawakaribisha sana.

1.0 UTANGULIZI

SCCULT (1992) Ltd ni chama Kikuu cha Ushirika wa Akiba na Mikopo Tanzania kilichoandikishwa upya mwaka 1992 kwa Sheria ya Ushirika namba 15 ya mwaka 1991 na kupewa hati ya usajili namba 5480. SCCULT (1992) Ltd ni kifupi cha Savings and Credit Cooperative Union League of Tanzania ambacho ni chama mwavuli kwa vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS) Tanzania Bara. Mojawapo ya shughuli ya SCCULT (1992) Ltd ni kutoa elimu, mafunzo na habari (kama msingi namba tano wa ushirika unavyoelekeza) kwa wanachama, viongozi, watendaji wa SACCOS na wadau wengine wa Ushirika wa Akiba na Mikopo. Kama ilivyosisitizwa kwenye msingi huo namba 5 (tano) wa ushirika pia SCCULT (1992) Ltd imeamua kuwekeza kwenye eneo hilo ili kuhakikisha kama Chama Kikuu tunachukua jukumu la kuboresha uelewa, mbinu, stadi kwa wanachama, viongozi na watendaji katika kutekeleza majukumu yao na kuhakikisha kuwa wanakuwa na mbinu za kisasa wakati wa kutimiza majukumu yao. Katika kuhakikisha kuwa huduma za mafunzo zinatekelezwa kwa ufanisi na tija, SCCULT (1992) Ltd tumeandaa mpango wa mafunzo kwa mwaka 2021 ukiwa na malengo yafuatayo;

1. Kuhakikisha kuwa Vyama vya ushirika wa akiba na mikopo vianaendelea kuelimishwa kuhusu ushirika kama dhana Mama na manufaa yake kwa wanachama.

2. Kuwa na viongozi walioelimika wenye kuwajibika na wenye uwezo wa kusimamia na kudhibiti kikamilifu shughuli za vyama vya Ushirka wa Akiba na Mikopo kwa manufaa ya wanachama na hivyo basi kutetea misingi na maadili ya ushirikiano kwa ustawi endelevu wa SACCOS.

3. Aidha katika mpango huu SCCULT (1992) Ltd imekusudia kuhakikisha kuwa elimu ya ushirika katika ngazi ya wanachama itazingatiwa lengo likiwa ni kuhakikisha kundi hilo kubwa na muhimu linaendelezwa na kufahamu mambo mbalimbali yanayohusu ushirika kwa ujumla, biashara ya ushirika wa fedha, mazingira ya Sekta ya ushirika na mambo mengine ambayo ni muhimu kwao. Msisitizo wa elimu utakuwa katika shughuli za kiuchumi zinazoendeshwa kiushirika, kazi na wajibu wa wanachama na manufaa ya kuwa mwanachama wa vyama wa Ushirika wa Ushirika wa Akiba na Mikopo.

1.1 Dira/ Maono ya SCCULT (1992) Ltd

Kuwa Taasisi ya kiushirika yenye nguvu na endelevu inayohamasisha na kuchangia upatikanaji wa huduma jumuishi za kifedha tanzania.

1.2 Dhamira/Dhima

Taasisi mwavuli iliyojikita kuhakikisha ustawi wa SACCOS tanzania kupitia utetezi, uzengezi na msaada wa kitaalamu

1.3 Kauli Mbiu

SCCULT jumuishi kwa ustawi wa SACCOS

1.4 Maadili

Maadili ambayo hutumika kuelekeza utendaji na utoaji huduma za kila siku;

(a) Weledi
(b) Timu/umoja
(c) Ubunifu
(d) Uwazi
(e) Uadilifu

2.0 KAZI NA WAJIBU WA SCCULT (1992) LTD

SCCULT (1992) Ltd katika kutimiza ndoto zake pamoja na dhamira ilizonazo itafanya na kutekeleza kazi zifuatazo;

i. Kutekeleza Mipango

Kutekeleza Majukumu ya kimipango yenye mitazamo ya kustawisha na kuzikuza SACCOS kwa kuzijengea uwezo wa kitaasisi na kifedha (Financial and Institutional capacity building) kwa kupatia viongozi na watendaji wa SACCOS elimu, maarifa na habari za ushirika.

ii. Uratibu

Kusimamia kwa karibu na kuratibu kwa usawa taratibu na uendeshaji wa shughuli za SACCOS hapa nchini na kuhakikisha kuwa taratibu za utunzaji wa kumbukumbu na mifumo ya utoaji wa taarifa mbalimbali za kifedha na takwimu inawiana kwa SACCOS zote bila kujali mifungamano yao.

iii. Utetezi

Kutoa utetezi na ushauri wa kitaalamu katika kusaidia SACCOS maeneo yenye vikwazo pindi watafutapo msaada au jambo lolote lile lenye maslahi kwa SACCOS na wanachama wake ikiwa ni serikalini au mamlaka mbalimbali mashirika na asasi za kijamii au za kifedha.

iv. Ushauri elekezi

Kushauri SACCOS mipango mizuri ya uwekezaji na fursa nyingine za kibiashara kwa kuzisaidia kuziunganisha na wataalamelekezi na kupata mitaji ya kuwekeza nje ya uwezo wao wa ndani.

v. Mafunzo na Ujenzi wa Uwezo

SCCULT (1992) Ltd inatoa mafunzo kwa wanachama, viongozi, watendaji wa SACCOS na wadau wengine wa ushirika wa akiba na mikopo. Mafunzo haya kutolewa kulingana na kalenda ya mafunzo ya SCCULT (1992) Ltd na mafunzo mengine huandaliwa mahususi kutokana na mahitaji maalumu ya SACCOS. SCCULT pia huandaa mafunzo mbalimbali kushirikiana na wadau mbalimbali wa SACCOS ili kuongeza ubora na ufanisi wa SACCOS.

3.0 AINA ZA MAFUNZO

3.1 Mafunzo ya Darasani

Mafunzo yatatolewa kwa mfumo wa utoaji wa semina, kuendesha makongamano na mikutano kwa kualika washiriki kufika katika eneo la mafunzo kufuatana na kalenda ya iliyotolewa, au SCCULT (1992) Ltd kualikwa kwenda kutoa mafunzo katika mikutano au makongamano ya watu wengine ikiwa pamoja na asasi na idara za serikali zenye nasaba na vyama vya Ushirika.

3.2 Mafunzo Kazini (On job trainings)

Aina hii ya mafunzo huendeshwa na SCCULT(1992) Ltd kwa kutumia kalenda yake ya mafunzo kuendesha semina ambayo SACCOS inahitaji lakini mafunzo hayo hayaendi sambamba na muda wala tarehe iliyoainishwa kwenye kalenda. Uongozi wa SACCOS uliopatiwa jedwali la mafunzo unaweza kuchagua mafunzo inayohitaji na kuwasiliana na SCCULT (1992) Ltd kukubaliana jinsi mafunzo hayo yatakavyoendeshwa. Mafunzo haya hufanyika katika sehemu za kazi kwenye SACCOS zenyewe (in-house trainings).

3.3 Mafunzo Maalumu (Taller made)

SACCOS huandaa mpango wake wa elimu na mafunzo na kuona kama baadhi ya maeneo katika mpango wao yanaoana na yale yaliyomo kwenye kalenda ya mafunzo ya SCCULT(1992) Ltd, basi hukubaliana na uongozi wa SACCOS namna ya kuendesha mafunzo hayo hii ni pamoja na yale ya darasani, kwenye mikutano au nje ya Nchi.

3.4 Mafunzo Shirikishi (Participatory)

Aina hii ya mafunzo hutolewa kwa hitaji la utekelezaji wa jambo fulani kwa mfano wanachama na wadau wameshauri SACCOS kuandaa mpango mkakati wa muda fulani. Katika eneo hili SCCULT(1992) Ltd itafanya kazi kama Mshauri Mwelekezi (Consultant) na kuendesha warsha maalum (Specific Training) ya kuandaa mpango mkakati kwa kuwashirikisha wadau muhimu wa SACCOS kuandaa mpango toka hatua ya utambuzi wa mpango hadi hatua ya mwisho ya kuwa na kijarida cha Mpango (Strategic document/Booklet).

3.5 Ziara za Kimafunzo ndani ya Nchi

Ziara ya kimafunzo ndani ya nchi inaweza kuandaliwa kwa SACCOS moja kutembelea SACCOS nyingine katika eneo lao, au kwa washiriki wa semina moja kutembelea SACCOS au eneo fulani kwa ajili ya kujifunza zaidi na kubadilishana maarifa na utaalam.

3.6 Ziara ya kimafunzo nje ya Nchi

Ziara ya kimafunzo nje ya nchi zinalenga kuhusisha wawakilishi wa SACCOS kutembelea nchi jirani kujifunza. Zoezi la ziara ya kimafunzo huendeshwa kwa kuchagua eneo fulani ambalo washiriki wataweza kutembelea na kuona kinachoendelea kwenye Ugani (Fiel) kwa kuoanisha nadharia ya darasani. Kwa mfano mada inaweza kuwa uwekezaji wa mifumo laini kwenye SACCOS baadaye mwezeshaji anaweza kupeleka washiriki kwenye SACCOS ambayo tayari imewekeza kwenye FOSA na kutumia mfumo laini na washiriki wakapata fursa ya kuona jinsi FOSA inavyofanya kazi na changamoto zake. Ziara ya kimafunzo nje ya nchi zinalenga kuhusisha wawakilishi wa SACCOS kutembelea nchi jirani kujifunza yafuatayo miongoni mwa mengi;

I. Utaratibu wa kutoza kodi kwenye SACCOS
II. Mchango wa Serikali katika kuendeleza SACCOS katika nchi hizo
III. Mchango wa SACCOS katika kukuza uchumi wa nchi husika
IV. Muundo wa Ushirika kisekta
V. Mgawanyo wa kazi wa wadau wa ushirika wa sekta ya Akiba na Mikopo

4.0 MBINU NA NJIA ZA UWEZESHAJI

Katika taratibu za utoaji elimu na mafunzo SCCULT(1992) Ltd katika programu yake itashirikisha wadau wa kuwezesha elimu ya ushirika wa Akiba na Mikopo kutoka wataalamu wake wa ndani ambao wana taaluma na uzoefu katika nyanja mbalimbali za elimu ya SACCOS. Aidha hushirikisha Vyuo vikuu, taasisi za watu binafsi na idara za Serikali ambao wana ujuzi wa mafunzo mbalimbali na wakati mwingine inashirikisha hata watu binafsi ambao nao ni wadau na wanauzoefu kwenye uwezeshaji wa biashara ya ushirika wa fedha. Kwa ujumla mbinu za ufundishaji hutumika kufuatana na aina ya mafunzo na washiriki wenyewe. Miongoni mwa mbinu hizo ni kama ifuatavyo;

4.1 Matumizi ya Darasa

Darasa hutumika kwa ajili ya kumuwezesha Mwalimu/Mwezeshaji kuendesha mafunzo akiwa kama mwalimu mbele ya darasa kuwasilisha somo kwa maana ya kuwapa nadharia. Mafunzo mengine yanahitaji zaidi ushirikishwaji kwa vitendo kama vile kozi za utunzaji vitabu, kuandaa makadirio nk.

4.2 Kazi za Vikundi

Aidha mijadala ya wazi hutumika kupia vikundi vidogo kwa kujibu swali moja kupata mawazo mengi ya washiriki au maswali tofauti tofauti na baadaye kujadili kwa pamoja katika darasa kubwa la washiriki, njia hii inaweza kutumika kuwajengea washiriki ufahamu zaidi na kubadilishana uzoefu miongoni mwao.

4.3 Michezo, Maigizo na visa mkasa

Hutumika hasa katika kuhamasisha uelewa wa washiriki katika jambo fulani na kufanya marejeo ya matukio hayo katika sehemu zao za kazi au katika jamii.

5.0 MATARAJIO

Baada ya zoezi la kutoa mafunzo kukamilika kutokana na kalenda ya mafunzo ambayo inaonesha idadi ya mafunzo, aina ya mafunzo na washiriki wa mafunzo. Malengo ya ushiriki katika kila darasa la mafunzo ni washiriki sabini (70) na ushiriki katika ziara za kimafunzo nje ya nchi ni washiriki 35. Inahisiwa kwamba mpango huu wa mafunzo hautaathiriwa na jambo lolote lile litakalotokana na kadhia ya mabadiliko ya kisiasa, uchumi, kijamii nk. Kwamba mipango ya wadau wote itatekelezwa ipasavyo na SCCULT (1992) Ltd itaendesha shughuli zake za kimafunzo kwa urahisi na ufanisi wa pekee hivyo basi matokeo tarajiwa ni pamoja na;

I. Wanachama na Bodi mpya na zinazoendelea za uongozi wa vyama vya ushirika wa akiba na mikopo zimepatiwa mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia tafiti, mitaala, miongozo, Sheria ya ushirika na Sheria ya huduma Ndogo za fedha na kanuni za SACCOS daraja la tatu . Wajumbe wa Bodi watakuwa na uwezo wa kuongoza na kusimamia shughuli za SACCOS zao.

ii. Watendaji mbalimbali wa vyama vya ushirika wa akiba na mikopo watawezeshwa katika maeneo yao ya kazi kwa kuwapa mbinu mpya na kuwakumbusha majukumu yao katika kutekeleza Sera na Mipango ya utoaji huduma na kuendeleza SACCOS zao kwa weledi na ujuzi unaostahili.

iii. Kamati za Bodi na kamati za usimamizi zitakuwa zimewezeshwa juu ya namna bora ya kutekeleza kazi na majukumu ili kuhakikisha wanachama wanaendelea kufaidi huduma ndani ya SACCOS zao kila wakati

6.0 TATHMINI YA MAFUNZO (Training Need Analysis)

Chama kikuu cha Ushirika wa Akiba na Mikopo Tanzania SCCULT (1992) Ltd kiliendesha zoezi la ukusanyaji wa maoni juu ya huduma zitolewazo. Lengo lilikuwa ni kupata taarifa zitakazosaidia kuboresha huduma bora za mafunzo na ushauri wa kitaalamu ili kusaidia kukabili changamoto ziliizopo katika utekelezaji wa shughuli za ujenzi wa uwezo wa kita-

asisi kwa vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS). Barua za uendeshaji wa zoezi la kufanya tathmini zilitumwa kwa vyama wanachama na wasio wanachama zikiwaomba wasidie kutoa maoni na mapendekezo. Wahusika walijaza fomu kwa namna mbili kuna waliojaza fomu na kuzirejesha ofisini moja kwa moja na kuna waliojaza fomu kwa kutumia simu janja/kompyuta , mchakato wa upembuzi wa maoni ulifanyika na kupelekea kupatikana kwa Kalenda ya mafunzo kwa mwaka 2021.

7.0 KALENDA YA MAFUNZO MWAKA 2021

Kalenda hii ni Mwongozo tu na sio wito wa kuhudhuria mafunzo au Semina, wito wa kuhudhuria semina hufanyika kwa barua maalumu za mialiko na hutumwa kwenye vyama ili kuwapa taarifa ili kuwawezesha kuteua na kutuma washiriki. Mialiko hutumwa kwa njia ya barua pepe, matangazo na baadae zoezi la kuwapigia simu, au meseji kwaajili ya ufuatiliaji. Kalenda ya mafunzo kwa kipindi cha kuanzia Mwezi Januari - Disemba 2021, imetolewa katika Jedwali maalumu ambalo limeambatanishwa kwenye Mpango wa Elimu na Mafunzo wa Mwaka 2021, jedwali kwa muhtasari kama ifuatavyo.

7.1 KALENDA YA MAFUNZO KWA MWAKA 2021 KWA VYAMA VYA USHIRIKA WA AKIBA NA MIKOPO

Na	SEMINA/ TUKIO	TAREHE YA SEMINA	UKUMBI/ ENEO	WALENGWA
1.	Mafunzo maalumu kwa Viongozi wapya wa Bodi kwa SACCOS na wale wanaoendelea. (Wajibu wa Viongozi katika utekelezaji wa Mipango kwa ufanisi na tija kwa Maendeleo na ustawi wa SACCOS Tanzania kwa mwaka 2021)	**Januari 19, 2021 - Januari 22, 2021**	MOROGORO KINGS WAY HOTEL	Viongozi wapya kwenye SACCOS watapewa kipaumbelea na wale wanaoendelea kwa kiasi
2.	Mafunzo maalumu kwa Viongozi wapya wa Bodi kwa SACCOS na wale wanaoendelea **(Mafunzo haya yatakuwa muendelezo wa Mafunzo ya Januari 19 – Januari 22, 2021 kama idadi ya washiriki itakuwa kubwa na kulazimika kufanya mafunzo haya kwa makundi mawili)**	**Februari 9, 20201 – Februari 12, 2021**	MOROGORO KINGS WAY HOTEL	Viongozi wapya kwenye SACCOS watapewa kipaumbelea na wale wanaoendelea kwa kiasi
3.	Mkutano wa tatu Shirikisho la Vyama vya ushirika wa akiba na Mikopo Afrika kwa ukanda wa Afrika Mashariki (ACCOSCA-EASTERN BLOCK REGIONAL MEETING)	**Februari 23 – Februari 26, 2021**	Dar es Salaam	1. Wanachama 2. Viongozi 3. Watendaji 4. Wadau wa ushirika wa akiba na mikopo
4.	Kikao cha pamoja cha Mameneja wa SACCOS Tanzania (Tanzania SACCOS Managers roundtable Meeting)	**Machi 17, 2021 – Machi 20, 2021**	Arusha	1. Mameneja
5.	Ukokotoaji wa riba za kiushindani na kibiashara kwa SACCOS pamoja na mbinu za udhibiti wa biashara na huduma za mikopo	**Aprili 20, 2021 – Aprili 23, 2020**	Dodoma	1. Kamati za mikopo 2. Mameneja 3. Maafisa Mikopo
6.	ZIARA YA KIMAFUNZO NDANI YA NCHI Vyama viwili maeneo ya Kazi na Vyama viwili vya kijamii Maeneo ya kujifunza (i) TEHAMA (ii) Utawala wa Mikopo (iii) Mbinu za kuongeza wanachama (iv) Huduma kwa wateja (v) Kuendesha Matawi kwa Ufanisi	**Mei 5, 2021 – Mei 7, 2021**	Kilimanjaro na Arusha	1. Wanachama 2. Viongozi 3. Watendaji

Na	SEMINA/ TUKIO	TAREHE YA SEMINA	UKUMBI/ ENEO	WALENGWA
7.	Uandaaji na uendeshaji wa vikao/Mikutano yenye tija kwa SACCOS	**Mei 25, 2021 – Mei 28, 2021**	Kanda ya Kaskazini (TANGA, KILIMANJARO, ARUSHA NA MANYARA)	1. Viongozi 2. Mameneja 3. Wakuu wa Idara
8.	**ZIARA YA MAFUNZO NCHINI KENYA** kujifunza (Study Tour) (i) FOSA (Front Office Service) (ii) Utawala wa mikopo (iii) Uwekezaji na Ubunifu wa Bidhaa (iv) Mbinu ya kuongeza wanachama na Mtaji (v) Kuji-brand kimkakati mawasiliano na kutengeneza muonekano bora (Strategic Branding Positioning, Communication and Corporate Reputation)	**Juni 09, 2021 – Juni 11, 2021**	Nairobi, Kenya	1. Wanachama 2. Viongozi 3. Watendaji
9.	**USHIRIKA MARATHON**	**18 Juni, 2021**	Moshi - Kilimanjaro	1. Wana Ushirika wote 2. Watanzania wote 3. Wadau wote
10.	Menejimenti Rasilimali watu kwa SACCOS (Sheria za ajira, taratibu za Mikataba, mahusiano na usuluhishi) pamoja na masuala ya manunuzi yanayofuata Sheria kwenye SACCOS	**Juni 22, 2021 – Juni 25, 2021**	Moshi, Kilimanjaro	1. Wajumbe wa Bodi 2. Kamati za ajira na elimu 3. Mameneja
11.	Maadhimisho ya siku ya Ushirika Duniani (SUD 2021)	**Julai 3, 2021**	Itataarifiwa	1. Wanachama 2. Viongozi 3. Watendaji 4. Wadau wote wa ushirika
12.	Utunzaji kumbukumbu na uendeshaji wa shughuli za Chama kwa Makarani na wasaidizi wa Ofisi za Vyama vya ushirika wa akiba wa mikopo	**Julai 20, 2021 – Julai 23, 2021**	Tanga	1. Makarani 2. Wasaidizi wa Ofisi
13.	Maadhimisho ya siku/wiki ya maonesho ya kilimo (Nane-Nane 2021)	**Agosti 01, 2021 – Agosti 08, 2021**	Simiyu	1. Wana ushirika wote watakao karibishwa
14.	Uboreshaji wa shughuli za ukaguzi na usimamizi kwa SACCOS	**Agosti 24, 20201 – Agosti 28, 2020**	Iringa	1. Kamati za usimamizi 2. Wakaguzi wa ndani

Na	SEMINA/ TUKIO	TAREHE YA SEMINA	UKUMBI/ ENEO	WALENGWA
15.	Kufanya tathimini za mahitaji ya wanachama na usimamiaji wa Kanuni za kumlinda mteja (mwanachama) kwa mujibu wa Sheria	**Septemba 21, 2021 – Septemba 24, 2021**	Bagamoyo	1. Viongozi 2. Mameneja
16.	Maadhimisho ya siku ya SACCOS Duniani (ICUD) na Mkutano mkuu wa 24 SCCULT(1992) Ltd	**i. Oktoba 18 – Oktoba 21, 2021 (ICUD 202)** **2. Oktoba 22, 2021** Mkutano Mkuu wa 24 wa SCCULT (1992) Ltd	Morogoro	1. Wanachama 2. Viongozi 3. Watendaji 4. Wadau wa ushirika wa akiba na mikopo 5. AGM ni kwaajili ya wanachama hai wa SCCULT (1992) Ltd tu
17.	Uandaaji na uendeshaji wa vikao/Mikutano yenye tija kwa SACCOS	**Novemba 10, 2021 – Novemba 12, 2021**	Kanda ya Nyanda za juu kusini (IRINGA, NJOMBE RUVUMA, MBEYA)	1. Viongozi 2. Mameneja 3. Wakuu wa Idara
18.	Uboreshaji wa huduma kwa kupitia TEHAMA	**Novemba 23, 2021 – Novemba 26, 2021**	Arusha	1. Maafisa TEHAMA
19.	Kupima na kutathmini utendaji na utekelezaji wa Mpango kazi kwa mwaka 2021 (Performance and Management Appraisal of Action plan for 2021)	**Disemba, 14 2021 - Disemba 17, 2021**	Dodoma	1. Wanachama

SACCOS BRINGS PEOPLE TOGETHER

SCCULT

The Savings and Credit Cooperative Union League of Tanzania
SCCULT (1992) LTD
CHAMA KIKUU CHA USHIRIKA WA AKIBA NA MIKOPO TANZANIA.
Mtaa wa Lumumba, Mnazi mmoja.
P.O. Box 20640 Dar es Salaam

Baruapepe: info@sccult.com
Tovuti: www.sccult.com
Simu: +255 222 185 548/9